TANGAZO LA SERIKALI Na…… la tarehe…201….

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA MAMLAKA ZA MIJI

SURA YA 288

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 89

SHERIA NDOGO ZA (KILIMO HIFADHI NA MAZAO YA CHAKULA) ZA HALMASHAURI YA MJI WA NZEGA ZA MWAKA 2016

Jina na mwanzowa kutumika	1.		Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Kilimo na Hifadhi za Mazao ya Chakula) za Halmashauri ya Mji wa Nzega za mwaka 2016 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.
Matumizi	2.		Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Mji wa Nzega.
Tafsiri	3.		Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:- **"Afisa Mwidhiniwa"** maana yake ni mtumishi yeyote atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi; **"Halmashauri"** maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Nzega; **"Kaya"** maana yake ni mume, mke, watoto pamoja na ndugu wanao ishi kwa pamoja; **"Mkazi"** maana yake ni raia wa Tanzania ambaye ama ana kaya au anaishi katika kaya au taasisii liyopo katika eneo la Halmashauri isipokuwa mtu ambaye:- (a) Ana umri wa miaka chini ya 18; (b) Hawezi kufanya kazi kwa sababu ya ugonjwa, au uzee au ulemavu. **"Mazao ya chakula"** maana yake ni Mahindi, Mtama, Maharage, Ulezi, Viazi, Kunde, Mpunga.
Wajibu wa	4.	(1)	Kila mkazi anayemiliki ardhi kwa mujibu wa sheria yeyote ile

Mkulima			atatakiwa kulima na kutunza shamba lisilopungua nusu ekari ya mazao ya chakula yanayostawi na kuhimili hali ya hewa na udongo was ehemu husika na kama itakavyoelezwa na Halmashauri.
		(2)	Kila mkazi atakaye lima shamba katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuvuna mazao yake pindi yakishakomaa na kuyahifadhi katika njia ya usafi ili kutunza ubora wake na kuhifadhi katika njia ya usalama.
		(3)	Litakuwa ni jukumu la kila mkazi hususani mkuu wa kaya kuhakikisha kuwa anahifadhi chakula cha kutosha yeye na familia yake kwa angalau mwaka mmoja au zaidi.
		(4)	Litakuwa ni jukumu la kila kaya kuwa na ghala la kuhifadhi chakula ambalo litapaswa kuwa katika hali ya usalama na lisiwe na uwezekano wowote wa kuruhusu wadudu kama vile dumuzi, panya au wadudu wengine wanaoweza kusababisha uharibifu wa chakula hicho.
Wajibu wa Halmashauri	6.		Halmashauri itakuwana wajibu wa:- (1) Kuhakikisha viongozi wa serikali, vyama vya siasa na wadau wengine wanashiriki ipasavyo katika kuendeleza sekta ya kilimo katika Halmashauri; (2) Kuunda vikundi vya sanaa vinavyohamasisha kilimo cha kisasa; (3) Kuwe bango kwenye kila kijiji yanayoeleza kanuni bora za kilimo yanayopaswa kuzingatiwa na mkulima kwa mazao yanayolimwa kwenye eneo hilo; (i) Kuanzisha shamba darasa ya mfano katika kila kijiji (ii) Kuhakikisha upatikanaji rahisi na kwa wakati wa pembejeo za kilimo. (4)Kutekeleza mipango ya msimu wa kilimo unaofuata mara baada ya mwisho wa msimu; (5)Kuhakikisha upatikanaji wa maafisa ugani katika kila kata au kijiji; (6)Kuhakikisha uanzishwaji wa vyama vya wakulima vya kuweka na kukopa kwa lengo la kujipatia mikopo ya benki; (7)Kuanzisha vituo vya kukuziana kufundishia wanyama kazi; (8)Kuanzisha vituo maalum kwa ajili ya kutolea mafunzo ya utumiaji na utunzaji wa zana bora za kilimo; (9)Kuhamasisha matumizi ya wafanyakazi katika maeneo ambayo wafugaji hujishughulisha pia na kilimo cha mazao; (10)Kushindanisha wakulima bora na maafisa ugani bora katika

			vijiji, kata na hatimaye Halmashauri; (11)Kuanzisha mfumo wa stakabadhi ya mazao; (12)Kuainisha matumizi bora ya ardhi galani ili kubainisha na kutofautisha ardhi ya mifugo, kilimo na hifadhi; (13)Kusimamia upatikanaji wa mbolea na pembejeo nyingine za kilimo; (14)Kusimamia upatikanaji, maadili na mwenendo wa mawakala wa mbolea na pembejeo za kilimo; (15)Kuhamasisha serikali za vijiji na wananchi kwa ujumla kujenga maghala ya chakula ya vijiji.
Wajibuwa Afisa Muidhiniwa	7.		Afisa mwidhiniwa atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba kila mkulima:- (1) Anaandaa mashamba kwa wakati; (2) Anapanda mbegu kwa mstari; (3) Anazingatia nafasi inayotakiwa kitaalam; (4)Anaweka mbolea kwa viwango na kwa wakati; (5) Anapalilia kwa wakati palizi mbili au zaidi.
Marufuku	8.	(1)	Ni marufuku kwa mtu yeyote kutengeneza pombe za kienyeji kwa kutumia mazao yaliyohifadhiwa kwa ajili ya chakula.
		(2)	Ni marufuku kwa mtu yeyote kung'oa, kuharibu au kusababisha uharibifu wa mazao yoyote yaliyolimwa na kutunzwa isipokuwa kwa madhumuni ya kilimo.
		(3)	Ni marufukuku kusafirisha mazao kuanzia saa 1:00 usiku
Wajibu wa Mkurugenzi	10.		Mkurugenzi anaweza kutoa maelekezo yanayohusu utunzaji wa mazao ya chakula baada ya kuvunwa kwa madhumuni ya kujikinga na njaa na kusimamia matumizi bora ya chakula katika Halmashauri.
Kosa	11.		Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi mitatu jela (3) au vyote viwili faini na kifungo.

Nembo ya Halmashauri ya Mji wa Nzega imebandikwa kwenye Sheria Ndogo kufuatia Azimio lilipoitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika Tarehe **…….**

……..

PHILEMON M. MAGESA

MKURUGENZI HALMASHAURI

MJI NZEGA

……

WILLIAM W.JOMANGA

MWENYEKITI HALMASHAURI

MJI NZEGA

Nakubali…….

Tarehe ……..

……..

MH.JOHN POMBE MAGUFULI

RAIS